

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO

## TAFSIRI RAHISI KWA WAWEKEZAJI KUHUSU MAZINGIRA WEZESHI

### NI HAYA YAFUATAYO:-

#### 1. KUWEPO KWA UONGOZI IMARA UNAOFUATA UTAWALA BORA WA KISHERIA.

#### 2. UKUBWA WA ENEO NA UWINGI WA WATU.

KUWEPO KWA ENEO KUBWA LA WILAYA AMBAPO NI KILOMETA ZA MRABA 16,685 NA IDADI YA WATU NI 244,669 KWA SENA YA KITAIFA YA MWAKA 2012

#### 3. WILAYA KUWA TULIVU

Kiteto ni mahali tulivu ambapo wananchi na wawekezaji mbalimbali waliopo wa ndani na nje ya Wilaya wanafanya kazi zao bila buguza yoyote.

#### 4. NAFASI YA KUVUTIA YA KIJIOGRAFIA

Kiteto ina nafasi ya nzuri sana ya kijiografia ambapo ni kichocheo muhimu cha kiuchumi na kibiashara kwa kupata wateja wa Wilaya na Mikoa ya jirani yaani Tanga, Arusha, Morogoro, ndani ya Mkoa pia wa Manyara na Makao Makuu ya Nchi yetu Dodoma.

#### 5. MIUNDOMBINU RAHISI YA USAFIRI KWENDA MIKOA YOTE NA NJE YA NCHI

Uwepo wa miundombinu safi ya uchukuzi mkubwa wa abiria na mizigo ndani ya nchi na nje ya nchi unaowezesha kuwafikia watu zaidi ya milioni 400, kama ifuatavyo:-

- usafiri wa anga kwani kuna jumla ya Viwanja Vidogo vya Ndege vipatavyo vitano navyo ni Loolera, Partimbo, Irkiushibour, Makame na Engang'oengare.
- usafiri wa barabara zinazopitika masaa 24 kwa 7 za wiki na kwa mwaka mzima ambazo ni barabara kuu za kufika Kiteto - Kibaya zipo tatu;
  - ✓ ya kwanza ni barabara kuu ya kwenda Mikoa ya Kanda Kusini Mashariki yaani Jiji la Tanga na Mkoa wa Kilimanjaro
  - ✓ ya pili ni barabara kuu ya kwenda Mikoa yote ya Kanda kaskazini yaani Jiji la Arusha, Mjini Babati Mkoa wa Manyara, Singida na mingineyo.
  - ✓ ya tatu ni barabara kuu ya kwenda Mikoa ya kanda ya Mashariki ya Pwani Kama vile Dar es salaam, Kanda ya Kati Dodoma na Nyanda za juu za kusini mwa Nchi yetu yaani Jiji la Mbeya na Mikoa mingine
  - ✓ hii yote inakupa fursa ya kufika Nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki, SADC na nchi jirani ya Kongo DRC, Kenya, Uganda kwa urahisi.

#### 6. HUDUMA ZA KIBENKI NA USHIRIKA

Kuna matawi ya benki kubwa Tanzania ambazo ni CRDB Bank, NMB Bank na POSTAL Bank kuna taasisi zingine za kifedha nazo ni FINCA International, ABC Bank, Bayport, Faidika na Tunakopesha.

- Hata hivyo fedha za Huduma ya Mitandao ya simu ipo kuanzia M-pesa, Tigo-pesa, Airtel Money na Halopesa
- Mawakala ya Benki za CRDB Fahari huduma, FINCA na NMB wapo
- Vyama vya Ushirika wa Mazao (AMCOS) 15, Vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) 21 - VICOBA 80.

#### 7. MAWASILIANO YA SIMU NA INTANETI

Yapo mawasiliano mazuri kwa njia ya simu na intaneti yanayopatikana kupitia Kampuni ya TTCL, Airtel, Vodacom, Zantel, Tigo na Halotel. Hadi sasa watu wakiwa mbali na Mji wa Kibaya - Kiteto wanaangalia TV hata kwa njia ya simu tambuzi (Smart Phone) kwa urahisi kabisa.

#### 8. MIUNDOMBINU RAHISI YA USAFIRI NDANI YA WILAYA

Uwepo wa miundombinu safi ya uchukuzi mkubwa wa abiria na mizigo ndani ya Wilaya ya Kiteto kama ifuatavyo:-

Kuna Kampuni binafsi za usafirishaji wa mizigo na abiria kutoka Stendi Kuu ya Wilaya kwa Mabasi yainayohudumia usafirishaji wa abiria kwa mabasi yaendayo nje ya Wilaya kama vile Mkoa wa Dar es salaam, Morogoro, Dodoma, Arusha, Babati - Manyara na Tanga.

Pia kuna usafiri wa ndani kwa gari ndogo yaani Daladala (Commuter Buses) kwenda Mji Mdogo wa Matui, Engusero, Dosidosi, Njoro, Kijungu, Sunya, Mbigiri, Mbeli na sehemu zingine nyingi.

Usafiri wa Taxi, Boda boda na gari zingine za kukodishwa kwa wafanyabiashara binafsi upo siku zote na usafirishaji wa ndege za kukodi.

**9. NYUMBA ZA KULALA WAGENI.**

Zipo nyumba nzuri za kulala wageni zenye vyumba vya kuvutia na kujitosherea (self contained room), Baa na mikahawa ya chakula yenye nyama choma inapatikana pia.

**10. UWEPO WA MINADA MIKUBWA INAYOAMINIKA NCHINI TANZANIA**

Uwepo wa Minada 7 kati ya hiyo minada 5 ni mikubwa yaani Dosidosi, Sunya, Matui, Laiseri na Kibaya ambayo imepelekea Wilaya ya Kiteto kuwa kinara na kimbilio la wafanyabiashara kutoka Tanzania nzima kuja kununua na kuuza mifugo yao hapa kwa faida kubwa.

